

ZIJUE MBINU ZA KUPATA ASALI BORA, NA KUKUZA UCHUMI WAKO KUPITIA UFUGAJI NYUKI

Tanzania ni moja ya nchi zilizoidhinishwa kuuza Asali katika mataifa ya Ulaya. Bei ya asali ya asili yenye ubora uliotibilishwa ni kubwa, na zaidi ya asilimia 90 ya ardhi ya Tanzania inafaa kwa ufugaji wa nyuki. Hivyo hii ni fursa muhimu!

- 1 Weka mizinga yako mbali na mashamba ya mazao ya kilimo yanayotumia viuatilifu**
- 2. Zalisha asali kwa Wingi.** Ili kuwavutia wafanyabiashara wakubwa kununua asali yako ni lazima uzalishe kwa wingi, angalau tani 20 hadi 100 kwa mwaka. Wazalishaji wadogo wanashauriwa kuunda umoja wa uzalishaji asali
- 3. Hakikisha unavuna asali iliyokomaa vizuri.** Wakati wa kurina, tenganisha masega meusi na yale yenye rangi ya goldi. Asali yenye rangi ya goldi inakuwa na mvuto zaidi sokoni
- 4. Uhifadhi:** Hifadhi asali katika chombo kisafi, kikavu na kisichoruhusu hewa kupita. Weka mbali na joto kali na epuka kuweka asali katika vyombo vilivyotumika kuhifadhi bidhaa nyingine kama petroli
- 5. Zingatia ubora:** Zingatia kuzalisha asali yenye ladha na harufu nzuri, na kiwango kidogo cha maji. Matumizi ya moto au madawa wakati wa kurina yanaharibu sana ubora wa asali.
- 6. Weka lebo yenye maelezo muhimu:** Jina, Aina ya Asali, Anuani ya mzalishaji; Chanzo cha asali mfano – mikoko, miombo, ukanda wa pwani; tarehe ya uzalishaji na uchakataji, ujazo
- 7. Viwango vya Uthibitishaji;** Zingatia kuzalisha asali inayokidhi viwango vilivyowekwa kimataifa ili kupata fursa ya kuiza nje ya nchi
- 8. Wekeza katika matumizi ya teknolojia:** Zingatia matumizi ya mizinga bora, vifaa bora vya kurina, kuchakata, kuhifadhi na kusafirisha asali yako



Mizinga ya kisasa



Asali iliyokomaa



Mizinga ya kisasa



Machini ya kuchakata asali unaotumiwa na wafugaji wadogo wa Nyuki - Tabora



Imeandaliwa na Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA) kwa Ufadhili wa Mradi wa Kuongeza Mnyororo wa Thamani ya Mazao ya Misitu Tanzania
Kwa Mawasiliano zaidi: Mkurugenzi Mtendaji; Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania (MJUMITA); S.L.P 21522 Dar-es-Salaam – Tanzania; tovuti: www.mjumita.org barua pepe: mjumitaorg@mjumita.org

Kwa ufadhili wa ushirikiano wa Tanzania na Finland

